NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Ridvan – 2016

Kwa Wabaha'í  wa Ulimwengu

Marafiki Wapendwa sana,

Kwa majilio ya Mfalme wa Sherehe, kipindi cha maandalizi kwa ajili ya Mpango ufuatao wa ulimwengu kimekamilika: sasa tunawaita marafiki wa Mungu kwenye kujifunga kwa miaka mitano mipya ya ujasiri, unuiaji na rasilimali.

Kikosi cha waaminifu wa Bahaú'llah kipo tayari. Mikusanyiko ya kiasasi iliyoitishwa ulimwenguni kote katika miezi ya hivi karibuni imetuma ishara za mfuatano za shauku ili kuanza shughuli hii kuu. Majukumu yaliyomo katika ujumbe uliotumwa kwenye makongamano ya Washauri tayari yanatafsiriwa katika mipango mahsusi ya utekelezaji. Miongo ya jitihada ya kishujaa imeitengeneza jumuiya na kujipatia kipimo kilichothibitika cha uwezo katika kulea ukuaji, ikiikomaza kwa ajili ya wakati huu. Miongo miwili ya mwisho, hasa, imechapuza kwa udhahiri ustadi huu uliosubiriwa kwa hamu kwa ajili ya uinukaji.

Katika kipindi hiki, uasili wa mfumo unaokua kwa ajili ya utendaji umewawezesha marafiki kuendelea kulea na kuboresha uwezo muhimu, ukiongeza matendo rahisi ya huduma mwanzoni, ukiongoza kwenye ruwaza za kueleweka zaidi za utendaji, ambazo kwa upande mwingine zilidai ukuzaji wa uwezo ambao bado tata zaidi. Kwa njia hii, mchakato wa mpangilio wa ukuzaji rasilimali watu na ujenzi wa jumuiya umeanzishwa katika maelfu ya klasta na, katika nyingi ya hizo, zinasonga mbele zaidi. Umakini haukutolewa pekee kwa muumini binafsi, au kwa jumuiya, au kwa asasi za Imani; washiriki wote watatu wasiotenganishwa katika mabadiliko ya Utaratibu mpya wa Ulimwengu wanasisimuliwa kwa nguvu za kiroho zinazoachiliwa kupitia ukunjukaji wa Mpango Mtakatifu. Dalili za ukuaji wao zinaonekana zaidi na zaidi: katika kujiamini kwamba waumini wasiohesabika wamepata kushiriki maelezo ya maisha ya Bahaú'llah na kujadiliana athari za Ufunuo Wake na Ahadi isiyo na kifani; katika makundi yaongezekayo ya roho ambazo, kama matokeo, zimevutiwa kwenye Hoja Yake na zinachangia kwenye upatikanaji wa muono Wake uunganishao; katika uwezo wa Wabaha'í na marafiki zao, kwenye ngazi ya umma kabisa ya jumuiya, kuelezea kinaganaga uzoefu wao wa mchakato wenye uwezo wa kubadili tabia na kujenga uwepo wa kijamii; katika idadi kubwa zaidi ya maana ya wale wenyeji kwenye nchi ambao, wajumbe wa asasi za Kibaha'í na mawakala, sasa wanaongoza shughuli za jumuiya zao; katika utegemezi, ukarimu, na kutoa kwa dhabihu kwenye Mfuko, muhimu sana kwa ajili ya uendelezaji endelevu wa Imani; katika uchanukaji wa uvumbuzi ambao haukuwahi kutokea wa mtu binafsi na matendo ya pamoja katika kusaidia shughuli za ujenzi wa jumuiya; katika shauku

ya roho nyingi sana zisizo na ubinafsi katika mwanzo wa ujana ambao wanaleta nguvu kubwa kwenye kazi hii, kimuonekano kwa kujihusisha na elimu ya kiroho ya vizazi vichanga; katika kuinua tabia za kiroho za jumuiya kupitia mikusanyiko ya mara kwa mara kwa ajili ya ibada; katika uinukaji katika uwezo kwenye ngazi zote za utawala za Kibaha'í; katika utayari wa asasi, mawakala, na watu binafsi kufikiri kwa muktadha wa mchakato, kusoma uhalisia wao wa karibu na kutathmini rasilimali zao katika mazingira wanamoishi, na kufanya mipango katika msingi huo; ambamo kwa sasa ni somo tendeshi la kawaida, ushauriano, utendaji, na tafakari ambavyo vimepalilia mkao wa silika wa kujifunza; katika utambuzi unaoongezeka kwa kinachomaanishwa kuleta matokeo kwenye Mafundisho kupitia matendo ya kijamii; katika uzidishwaji wa fursa zitafutwazo na kuchukuliwa kutoa mtazamo wa Kibaha'í kwenye mijadala inayoendelea katika jamii; katika utambuzi wa jumuiya ya ulimwengu kwamba, katika juhudi zake zote, inaharakisha utokezaji wa ustaarabu mtakatifu kwa kudhihirisha nguvu ya ujenzi wa jamii iliyomo ndani ya Hoja; kwa kweli, ndani ya ufahamu wa marafiki kwamba juhudi zao za kukuza mabadiliko ya ndani, kupanua duara la umoja, kushirikiana na wengine katika uwanja wa huduma, kusaidia idadi za watu kuchukua wajibu wao katika ukuaji wa kiroho, kijamii, na kiuchumi – na, kupitia juhudi zote hizi, kuleta hali njema ya ulimwengu – huelezea kusudi lenyewe hasa la dini.

Wakati hakuna kipimo kimoja kinachoweza kukamata ujumla wa maendeleo ya jumuiya ya Kibaha'í, mengi yaweza kuonwa kutokana na idadi ya klasta kote ulimwenguni ambako programu za ukuaji zimeanzishwa, ambazo, kwa shukrani kwa ajili ya neema zilizojaliwa na Uzuri wa Abha, tunathibitisha zimevuka elfu tano. Msingi mpana sana kama huu ulikuwa kwa ajili ya kubeba jukumu ambalo sasa linaukabili ulimwengu wa Kibaha'í – kuimarisha mchakato wa ukuaji katika kila klasta ambamo ulianza na kupanua zaidi ruwaza itajirishayo ya maisha ya jumuiya. Juhudi endelevu inayohitajika itakuwa nguvu zaidi. Lakini matokeo yana uwezekano kuwa ya maana kubwa sana, hata kuweka kipindi cha historia. Hatua ndogo ndogo, zikiwa za mara kwa mara na za haraka, huongeza kwenye umbali mkubwa ulioendeka. Kwa kumakinikia kwenye upigaji hatua ambao lazima ufanyike katika klasta katika kipindi cha mwanzoni – mathalani, katika duru sita zitakazotokea kabla ya kumbukumbu ya kwanza ya kumbukumbu za miaka mia mbili – marafiki watafanya mengi kuleta lengo lao kwa ajili ya miaka yote mitano kukaribia kulifikia. Katika kila duru zimewekwa fursa zinazopita kwa ajili ya kusonga mbele, uwezekano wa thamani kubwa ambao hautajirudia.

Katika jamii kwa ujumla, ole, dalili za kuzidi kunyong'onyea kwa roho zinazidishwa na kuwa mbaya zaidi. Ni jinsi gani inagonga kwamba, vile watu wa ulimwengu wanavyoteseka kwa uhitaji wa tiba ya kweli na kugeuka wazima wazima kutoka tumaini moja lisilo la kweli hadi lingine, kwa pamoja mnaboresha chombo ambacho huunganisha mioyo na Neno la Mungu milele. Ni jinsi gani inagonga kwamba, katikati ya sauti kali zinazohitilafiana za mawazo mgando na maslahi yanayopingana ambayo huchipuka kila mahali kwa ukali zaidi, mnamakinikia juu ya kuwaleta watu pamoja ili kujenga jumuiya ambazo ni makimbilio ya umoja. Mbali na kuwakatisheni tamaa, acha chuki za kiulimwengu na uhasama viwe ukumbusho wa jinsi gani kwa haraka roho ziwazungukazo huhitaji mafuta ya uponyaji ambayo nyinyi pekee mnaweza kuyawasilisha kwao.

Hii ni ya mwisho katika safu ya mfuatano wa Mipango ya Miaka Mitano Mitano. Kwenye hitimisho lake, awamu mpya katika ukuaji wa Mpango Mtakatifu itafunguka, ikiwa imejipanga kupeperusha jumuiya ya Baha'u'llah kuelekea karne ya tatu ya Kipindi cha Kibaha'i. Acha marafiki wa Mungu katika kila nchi watambue ahadi ya miaka hii michache iliyo mbele, ambayo itakuwa maandalizi makali kwa ajili ya kazi kubwa zaidi ambayo bado inakuja. Upeo mpana wa Mpango wa sasa unamwezesha kila mmoja kusaidia kazi hii, hata mchango wa mtu uwe mdogo kiasi gani. Tunawaomba nyinyi, watendakazi wenzetu wathamaniwao, mumhusuduo Yule Ambaye ni Mpendwa Sana wa malimwengu, kutobakisha juhudi yoyote katika kutumia yote mliyojifunza na kila uwezo mliopewa na Mungu na ujuzi mlionao kuendeleza Mpango Mtakatifu kuelekea hatua yake muhimu ifuatayo. Kwenye maombi yenu ya shauku kwa ajili ya msaada wa mbinguni tunaongeza yetu, yanayotolewa kwenye Makaburi Matakatifu, kwa niaba yenu wote mnaoshughulika kwa ajili ya Hoja hii ikumbatiayo wote.

*UMESAININIWA NA NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU*